# HOTUBA YA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI, MHESHIMIWA AL-HAJJ DK. ALI MOHAMED SHEIN, KATIKA BARAZA LA IDD - EL- HAJJ, TAREHE 12 AGOSTI, 2019 MILADIA SAWA NA MWEZI 10 MFUNGUO TATU, 1440 HIJRIA.

**BISMILAHI RAHMANI RAHIM**

**Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan;**
**Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**

**Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi;**
**Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar,**

**Mheshimiwa Dk. Amani Abeid Karume;**
**Rais Mstaafu wa Zanzibar,**

**Mheshimiwa Khamis Juma Maalim;**
**Waziri wa Katiba na Sheria,**

**Mheshimiwa Omar Othman Makungu;**
**Jaji Mkuu wa Zanzibar,**

**Mheshimiwa Mgeni Hassan Reli,**
**Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar,**

**Mheshimiwa Khamis Haji Khamis;**
**Kadhi Mkuu wa Zanzibar,**

**Mheshimiwa Sheikh Mahmoud Mussa Wadi;**
**Naibu Mufti wa Zanzibar,**

**Waheshimiwa Mawaziri na Wajumbe wa BLM na Manaibu Mawaziri**

**Dk. Abdulhamid Yahya Mzee;**
**Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi,**

**Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi,**

An evaluation version of novaPDF was used to create this PDF file.
Purchase a license to generate PDF files without this notice.

**Dk. Abdalla Juma A. Saadalla;**
**Naibu Katibu Mkuu wa CCM - Zanzibar,**

**Mheshimiwa Ayoub Mohammed Mahmoud;**
**Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi,**

**Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya zote mliohudhuria,**

**Wakuu wa Vyombo ya Ulinzi na Usalama.**

**Viongozi wa Vyama vya Siasa.**

**Wageni Waalikwa.**

**Ndugu Wananchi.**

**Mabibi na Mabwana.**

**Assalamu Aleikum Warahmatullahi Wabarakatuh**

**IDD MUBARAK**

Sifa njema zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyeumba mbingu na ardhi na vyote viliyomo ndani yake na kwake Yeye ndio marejeo yetu sote. Mwenyezi Mungu kwa rehema na shani yake ameturuzuku neema ya uhai na afya njema tukaweza kuishuhudia sikukuu hii ya Idd ul- Adh'ha, leo tarehe 12 Agosti, 2019 Miladia, sawa na mwezi 10 Mfunguo Tatu, 1440 Hijria.

Tuna wajibu mkubwa wa kumshukuru Mola wetu kwa kutupa neema hizi na nyenginezo, tukizingatia kwamba kuna ndugu zetu Waislamu na wengineo ambao leo hii hawapo tena hapa duniani, kwani wamekwishatangulia mbele ya haki. Tumuombe Mwenyezi Mungu awape malazi mema ndugu, jamaa, marafiki na Waislamu wote waliokwisha tangulia mbele ya haki. Vile vile, awape shifaa wagonjwa wote kwa baraka za siku hii. Amin.

An evaluation version of novaPDF was used to create this PDF file.
Purchase a license to generate PDF files without this notice.

**Ndugu Wananchi,**

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia salama tukaweza kujumuika na wananchi wenzetu wa Mkoa huu wa Mjini Magharibi katika kuisherehekea sikukuu ya Idd-el-Hajj. Tuna furaha kubwa ya kupata nafasi ya kuwa pamoja katika uwanja huu maarufu wa Langoni - Kizimbani. Waislamu wenzetu Mahujaji kutoka katika mataifa mbali mbali, wapo katika Mji Mtukufu wa Makka huko Saudi Arabia; wakiwa na furaha na shukrani nyingi kwa Mola wetu, baada ya kuitekeleza ibada ya Hijja. Kwa hivyo, na sisi kwa upande wetu tupo hapa kwa ajili ya kuungana nao katika kuonesha furaha na kutoa shukrani hizo kwa Mola wetu Mtukufu. Kwa hivyo, wananchi wote wa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jumla, tunaungana na wenzetu ulimwenguni kuiadhimisha Sikukuu ya Idd-el Hajj.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa Uongozi wa Kamati ya Maandalizi ya Kitaifa ya Sherehe hizi kwa matayarisho yao mazuri. Kadhalika, natoa shukurani na pongezi kwa uongozi na watendaji wa Mkoa wa Mjini Magharibi na Wilaya ya Magharibi "A" kwa kushirikiana vyema na Kamati ya Maandalizi na yakapatikana mafanikio haya tunayoyaona. Kwa namna ya pekee, natoa shukurani kwa wananchi wote wa Mkoa huu kwa mapokezi mazuri na kwa kuwa pamoja nasi, tangu asubuhi katika sala ya Idd-el-Hajj tuliyosali katika viwanja vya Beit el Raas, na hivi sasa tumeungana tena pamoja katika Baraza hili la Idd. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie umoja, mapenzi na mshikamano na aujaze kheri na baraka mkusanyiko huu. Amin.

**Ndugu Wananchi,**

Kama tunavyoelewa kwamba Waislamu tumeamrishwa kufanya ibada mahali popote penye kukidhi masharti ya ibada inayohusika. Hata hivyo, ibada ya Hijja imepangiwa mahali pake maalumu ambapo masharti yake hayatimii ila mtu afike mahali hapo na afuate taratibu na miongozo yake. Mwenyezi Mungu ametuthibitishia hili katika kitabu chake cha Quran, katika aya ya 96 ya Surat Aali Imran kwa kutubainishia sifa za utukufu wa mahali hapo kwa tafsiri isemayo:

An evaluation version of novaPDF was used to create this PDF file.
Purchase a license to generate PDF files without this notice.

***"Kwa yakini Nyumba ya kwanza iliyowekwa kwa ajili ya watu kufanya ibada, ni ile iliyoko Makka, yenye baraka na uwongozi kwa ajili ya walimwengu wote".***

Na katika aya 97 ya Sura hio hio, tunaendelea kuelezwa kwa tafsiri isemayo kwamba:

***"Humo mna ishara zilizo wazi za kuonyesha utukufu wake na ukongwe wake. Miongoni mwa hizo ni mahali alipokuwa akisimama Ibrahim, na anayeingia (nchi hiyo) anakuwa katika salama (amani)".***

Kwa hivyo, kwa ndugu zetu kwenda kufanya ibada katika nyumba hii tukufu, Mwenyezi Mungu ameahidi kuwa watapata baraka za nyumba hio pamoja na uwongofu. Kadhalika, kwa kuwepo kwao katika Mji Mtukufu wa Makka wataweza kuzuru maeneo muhimu ya historia ya Uislamu zikiwemo sehemu ambazo Mtume wa Mwenyezi Mungu kama vile, Nabii Ibrahim alisimama. Fursa hio, imeahidiwa na Mwenyezi Mungu kuwa ni ya salama na amani.

**Ndugu Wananchi,**

Katika kuonesha thamani ya Mahujaji wetu miongoni mwa Waislamu, imepokelewa hadithi kutoka kwa Imam Ja'far Sadiq (A.S) ambaye ni miongoni mwa watu wa nyumba ya Mtume wetu Muhammad (SAW), kwamba Mtume huyo wa Mwenyezi Mungu (S.A.W) amesema:

***"Watu wanaofanya Hijja au Umra ni wageni wa Mwenyezi Mungu. Kama watakuwa na haja atawakidhia, na kama watamuomba atajibu maombi yao, na iwapo watanyamaza wasimuombe chochote, basi yeye Mwenyezi Mungu atawapa bila ya wao kumuomba".***

Kwa hakika, sote ni wahitaji kwa Mwenyezi Mungu, lakini Mahujaji wetu wataruzukiwa neema nyingi kwa kuwa ni wageni maalumu wa Mwenyezi Mungu. Vile vile, Mola wetu atawalipa, hata bila ya kumuomba, kwa vile tu wameamua kwenda

An evaluation version of novaPDF was used to create this PDF file.
Purchase a license to generate PDF files without this notice.

Hijja. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awafanyie wepesi Waislamu wote ambao bado hawajatekeleza ibada ya Hijja, ili na wao waweze kupata manufaa hayo makubwa yanayotokana na malipo yake Allah Subhanahu Wa Taala. Tunamuomba Mola Wetu awape uwezo zaidi Waislamu waliokwishawahi kwenda kufanya ibada ya Hijja na wanaotaka kwenda tena kufanya ibada hio.

**Ndugu Wananchi,**

Tukiwa tunasherehekea kukamilika kwa utekelezaji wa ibada ya Hijja, ni wajibu wetu tutafakari kwa makini mafundisho yanayoambatana na ibada hii. Ingawa Hijja ni ibada ya mara moja kwa mwaka na kwenye umri wa Muislamu ambaye hamudu kurejea mara nyengine, lakini utekelezaji wake unajumlisha mtiririko wa vitendo vya ibada kadhaa hadi kukamilika kwake. Ibada inatanguliwa na utii katika kuitikia wito wa Mola wetu na nia thabiti ya kuwajibikaji kwake. Kadhalika, ili mtu aweze kuwajibika vyema anahitaji kuwa na afya njema na fedha alizozichuma au kuzipata kwa njia za halali, ambazo zitamtosheleza kuzitumia kwa shughuli za Hijja pamoja na kuikimu familia yake, wakati atakapokuwa mbali nao katika utekelezaji wa ibada hio.

**Ndugu Wananchi,**

Uislamu umeweka mifumo mizuri ya kuendesha maisha yetu. Kwa kila ibada tuliyoamrishwa tuifanye, ni wajibu wetu tuifahamu vizuri mantiki na mafunzo tunayoyapata ambayo yatatuwezesha kuuendeshea mfumo wetu mzima wa maisha kwa ufanisi. Kutokana na hayo niliyoyaeleza, kuhusu ibada ya Hijja, tunajifunza kwamba utekelezaji wa kazi zetu za maendeleo kwa maslahi yetu unahitaji tuwe watiifu wa sheria juu ya mambo tunayotakiwa tuyafanye, pamoja na nia ya uwajibikaji kwa wale tunaowatumikia. Sambamba na hayo, tunahitaji tuwe na afya njema, na katika utekelezaji wa wajibu wetu chochote tunachokichuma tunapaswa tufahamu kuwa kitu hicho kiwe ni chumo la halali katika kutuendeshea maisha yetu na familia zetu.

Kama tunavyoelewa kwamba ibada ya Hijja inahitaji muumini aondoke nchini pake aende mahali mahsusi inakofanyiwa ibada hio, yaani Makka na huko muumini anahitaji ajiamini, awe mkakamavu na mwenye kufanya kila kitendo cha ibada kwa

An evaluation version of novaPDF was used to create this PDF file.
Purchase a license to generate PDF files without this notice.

wakati bila ya kuchelewa, kwa sababu akichelewa muda haumsubiri, ataachwa nyuma na lengo lake la kufanya ibada litakuwa hajalifikia.

**Ndugu Wananchi,**

Hapa tunajifunza kwamba, ili tuweze kuyafikia malengo ya maendeleo yetu kuna mambo ambayo hatuwezi kuyapata tu kwa kukaa ndani ya ofisi zetu au majumbani, ni lazima tuyafuate huko yaliko. Huko tunakoyafuata inatubidi tuyachangamkie kwa wakati na kujiamini. Tafakuri nyengine ya mafundisho ya ibada ya Hijja ni uvumilivu, subira na mshikamano. Mahujaji wanaotoka nchi mbali mbali, wenye utamaduni, tabia na silka tafauti, wanakusanyika pamoja na wanafanya ibada zao katika vituo mbali mbali kwa pamoja, lakini wanavumiliana, wanajenga subira ya hali ya juu. Kadhalika, Mahujaji wanashikamana wote kwa pamoja katika kufuata sheria na taratibu zilizowekwa wakiwa na lengo moja tu, nalo ni la kufanikiwa katika kuitikia wito wa Mola wetu. Hali hii inatuthibitishia kwamba suala la kuvumiliana, kujenga mshikamano na subira ni nyenzo kuu katika kuufikia ufanisi wa utekelezaji wa shughuli zetu za kila siku, kwa maslahi ya nchi yetu na sisi wenyewe.

**Ndugu Wananchi,**

Jambo jengine tunalojifunza kutokana na ibada ya Hijja ni umuhimu wa watu kufanya kazi zenye manufaa kwa njia ya kujitolea hata ikiwa wana hali duni. Suala hili linabainika katika aya ya 27 ya Suratul Hajj ambayo Mwenyezi Mungu anamuagiza Nabii Ibrahim (A.S) kwa kusema:

> ***"Na (tukamwambia) "utangaze kwa watu habari za Hijja, watakujia (wengine) kwa miguu na (wengine) juu ya kila mnyama aliyekonda (kwa machofu ya njiani wakija kutoka katika kila njia ya mbali."***

Nabii Ibrahim (A.S) alijitolea kufanya kazi ya kutangaza habari za Hijja kama alivyotakiwa na Mwenyezi Mungu bila ya kutajiwa kiasi cha malipo, ingawa bila ya shaka malipo yake anayajua Mwenyezi Mungu Mtukufu. Katika hali zetu sisi, kazi za kujitolea za maendeleo zina faida mbili, ambapo ya kwanza ni yale manufaa tunayoyapata na vizazi vyetu kutokana na kazi hio. Kwa mfano, tunapojitolea katika kusaidia kuimarisha huduma za jamii, faida ni yetu sote; lakini vile vile vitendo vizuri

An evaluation version of novaPDF was used to create this PDF file.
Purchase a license to generate PDF files without this notice.

huwa havikosi ujira kutoka kwa Mwenyezi Mungu; kama alivyotueleza katika Surat An- Nisaa, aya ya 40 yenye tafsiri isemayo:

> **"*Hakika Mwenyezi Mungu hawadhulumu (viumbe vyake hata kitu kilicho sawa na) uzito wa mdudu chungu; na kama likiwa ni jambo jema (Yeye Mungu) atalizidisha na kutoa ujira mkubwa unaotoka kwake.*"**

**Ndugu Wananchi,**

Inatupasa tufahamu kwamba utiifu wa amri zinazojenga utawala bora ni jambo lenye umuhimu mkubwa. Tunapotekeleza amri huwa tunafuata taratibu za utawala bora na amri hizo zinatokana na sheria tulizozitunga sisi wenyewe. Kadhalika, katika kutii amri na kufuata sheria, hakuna aliye juu kuliko mwengine. Mwenyezi Mungu Mtukufu katuonesha haya katika Quran, jinsi alivyompa mtihani Nabii Ibrahim (A.S) kwa kumtaka amchinje mtoto wake wa pekee Ismail, ambaye alimpata uzeeni na jinsi Nabii Ibrahim na mwanawe Ismail walivyokuwa tayari kuitekeleza amri ya Mwenyezi Mungu, kama Quran inavyotuelezea tukio hilo. Lakini mapenzi na huruma ya mtoto wake hayakumzuia Nabii Ibrahim (A.S) kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu na hata utamu wa maisha haukumshughulisha Ismail, akaamua kukubaliana na baba yake katika kutii amri ya Mwenyezi Mungu.

**Ndugu Wananchi,**

Tunasikia vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia katika jamii yetu, hasa vitendo viovu vya ubakaji wanaofanyiwa watoto wadogo, ambao hawana wanalolijua. Wakati mwengine uovu huo unahusishwa na watu wa familia, ambao waliobainika wafikishwe mbele ya sheria, ili haki itendeke. Kinachoshangaza ni kwamba mapenzi na huruma juu ya watu hao waovu hutawala ndani ya familia na inafika hadi familia hio huwaficha watu hao na kuiacha haki ya waliodhalilishwa ipotee. Tabia hii ni mbaya na inachukiza katika jamii yetu na hata mbele ya Mwenyezi Mungu. Lazima familia zielewe umuhimu wa kutii amri na kuwafikisha wahalifu wanaobainika mbele ya sheria, ili haki itendeke na uovu huu hatimae umalizike.

An evaluation version of novaPDF was used to create this PDF file.
Purchase a license to generate PDF files without this notice.

Ibada ya Hijja ni chuo chenye kutoa mafunzo na kumuongezea Muumini upeo wa uchamungu na kuitakasa nafsi yake kutokana na maovu. Muumini anaporudi kutoka kwenye ibada hii huwa ni mithili ya mtu aliyezaliwa upya. Huwa amejengeka katika akhlaki na mwenendo mwema uliojaa subira na uvumilivu. Huwa ni mwenye kujichunga sana katika kauli na vitendo vyake. Vile vile, tunaelezwa kuwa, katika msimu wa kutekeleza ibada ya Hijja, amani hutanda katika miji mitukufu na kubaki salama kwa wenyeji pamoja na wageni na viumbe wengine kama miti na wanyama.

Kwa hivyo, nawahimiza mashekhe, walimu na maulamaa wetu muendelee kushirikiana na waumini waliokwishahiji ambao wamefungamana na uchamungu, mjenge mshikamano imara utakaoendelea kuielimisha jamii yetu kuishi kwa amani, utulivu na kuheshimiana, ili jamii yetu iondokane na vitendo viovu vya uvunjaji wa sheria, tuweze kupata mafanikio zaidi.

**Ndugu Wananchi,**

Kwa hakika bila ya amani hatuwezi kupata maendeleo yoyote na wala waumini hatutaweza kupata wasaa wa kufanya ibada kwa utulivu. Tunayasikia matukio mbali mbali ya kusikitisha yanayotokea katika mataifa mengine, ambako amani imekosekana. Yanayotendeka huko ni vurugu, udhalilishaji na ukatili wa kila aina. Waumini wenzetu wamo ndani ya fadhaa, hawana maendeleo, hawana hata utulivu wa kufanya ibada, ili waweze kuungana na wenzao katika kusherehekea sikukuu mbali mbali. Tumuombe Mwenyezi Mungu awaondolee mtihani huu.

**Ndugu Wananchi,**

Tumshukuru Mola wetu Mlezi kwa kutujaalia kuwa na amani katika nchi yetu, nami kila nikipata nafasi ya kuzungumza nanyi wananchi wenzangu, nimekuwa nikisisitiza juu ya umuhimu wa kuendelea kuidumisha amani. Hakuna mbadala wa amani. Amani ni miongoni mwa baraka ambazo Allah Subhanahu Wa Taala ametupa nchini mwetu; na hivyo tunapaswa tuitunze kwa hali zote. Tutakapokuwa tunaitunza amani yetu, itakuwa tunaonesha shukrani kwa Allah kwa kutupa baraka hio. Kwa hakika iwapo tutakuwa tunaichezea amani kwa kujihusisha na vitendo vya uvunjaji wa

An evaluation version of novaPDF was used to create this PDF file.
Purchase a license to generate PDF files without this notice.

sheria, itakuwa tunaikufuru neema tuliyopewa; na Mola wetu Muumba anaweza kutuadhibu. Mwenyezi Mungu atuepushe na hilo.

Tunajifunza katika Uislamu pale ambapo Mwenyezi Mungu anatutanabahisha kwa mfano wa jamii iliyopewa neema ya amani na utulivu na ikashindwa kuitunza neema hio. Mfano huu tunaukuta katika Suratun Nahl, aya ya 112, yenye tafsiri inayosema:

> **"*Na Mwenyezi Mungu anakupeni mfano wa mji uliokuwa na amani na utulivu, riziki yake ikiujia kwa wingi kutoka kila mahali. Lakini ukazikufuru neema za Mwenyezi Mungu, kwa hivyo Mwenyezi Mungu akauvika vazi la njaa na khofu kwa sababu ya yale waliyokuwa wakifanya*"**

Ni wajibu wa kila mmoja wetu aizingatie aya hii kwa makini kutokana na kuuona umuhimu wa amani na utulivu kwa maisha na maendeleo yetu.

**Ndugu Wananchi,**

Kutokana na kuendelea kuwepo kwa amani na utulivu, nchi yetu inaendelea kupiga hatua na kuimarika kwa uchumi wetu kila mwaka. Hali hii inaiwezesha Serikali kupata nguvu zaidi za kuimarisha miundo mbinu ya uchumi na kutoa huduma mbali mbali, ambazo wananchi wanazihitaji kwa ajili ya maisha ya kila siku katika hali iliyo bora zaidi. Aidha, ukuaji huo wa uchumi umeiwezesha Serikali kuimarisha maslahi ya wafanyakazi wa Serikali na kuinua kipato chao pamoja kupata uwezo wa kuitekeleza mipango mbali mbali wanayojipangia.

Ni jambo la faraja kuona kuwa, hali hii vile vile, imewawezesha baadhi ya watumishi kupata uwezo wa kifedha kwenda kutekeleza ibada ya Hijja mapema, badala ya kusubiri fedha za kiinua mgongo kama ilivyozoweleka. Taarifa kutoka Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana zinaeleza kuwa, jumla ya Watanzania 2,500 walijitokeza mwaka huu kwa ibada ya Hijja, wakiwemo watu 1,700 kutoka Taasisi 22 za Zanzibar zinazoshughulikia masuala ya Hijja na watu 800 kutoka Taasisi za Tanzania Bara.

An evaluation version of novaPDF was used to create this PDF file.
Purchase a license to generate PDF files without this notice.

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwawezesha ndugu zetu hawa kwenda kuitekeleza ibada hio. Kwa hakika si kila aliyejaaliwa kupata neema hizo hudiriki kwenda kuitekeleza ibada hio kubwa. Kwa hivyo, nawahimiza waumini wenzangu wenye uwezo wa kifedha na afya njema kuepukana na vipingamizi visivyo na msingi ambavyo vinaweka usiri wa kwenda kuitekeleza ibada ya Hijja.

Hadithi za Mtume Muhammad (SAW) zinazozungumzia ibada ya Hijja zinamuhimiza kila mwenye uwezo kufanya haraka ya kutimiza wajibu huo. Katika kuthibitisha hilo, imepokelewa kutoka kwa Sayyidna Abdulla Ibn Abbas (R.A) kwamba Mtume wetu Muhammad (SAW) ametuusia kwamba:

> ***"Mwenye kutaka kwenda Hijja, basi afanye haraka, kwani anaweza kupata maradhi, au akapotelewa na uwezo wa fedha za kufanyia safari, au akazuiliwa na dharura itakayomnyima nafasi ya kwenda (Hijja)."***

Tufahamu kuwa wenye kuipata fursa ya kwenda kutekeleza ibada ya Hijja, na wakaitumia ipasavyo, huwa wamejiandalia hadhi mahsusi mbele ya Mwenyezi Mungu na wanapata fadhila kubwa kutokana na kufanya uwamuzi huo, kama inavyoelezwa katika aya ya 274 ya Suratul Baqarah yenye tafsiri isemayo:

> ***"Wale watoao mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhahiri, wana ujira wao kwa Mola wao wala haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika".***

Kauli hii ya Mwenyezi Mungu inawabashiria kheri ndugu, marafiki, jamaa na Waislamu wote ambao wameamua kutoa fedha zao kwenda kuitekeleza ibada ya Hijja. Ni jambo la kufurahisha sana kuona kwamba idadi ya Waislamu wanaosaidia Waislamu wengine kutekeleza ibada hiyo imekuwa ikiongezeka. Watu wanaosaidia katika mambo ya kheri bila ya shaka, wana ujira mwema mbele ya Allah Subhanahu Wa Taala kama ilivyothibitika katika aya hiyo. Kwa hivyo ni wajibu wetu tuhimizane, ili wale wenye uwezo wawasaidie Waislamu wengine kwenda kufanya ibada hio kwa kuzingatia miongozo ya dini iliyopo.

An evaluation version of novaPDF was used to create this PDF file.
Purchase a license to generate PDF files without this notice.

Kadhalika, natoa shukurani kwa Taasisi zote zilizowahudumia mahujaji wetu. Vile vile, natoa shukurani kwa Taasisi ambazo zinawahamasisha Waislamu kwenda kutekeleza ibada hio na hasa zile ambazo huwasadia Waumini kuweka fedha na kuchangia kidogo kidogo hadi zinapotimia, wende wakahiji. Ni dhahiri kuwa mtindo huu unathibitisha kauli ya wazee kuwa *"Haba na haba hujaza kibaba*". Tumuombe Mwenyezi Mungu atupe uwezo zaidi wa kwenda kuitekeleza ibada hii na hasa kuufanikisha utumiaji wa Mfuko wa Hijja Zanzibar, ili watu wengi zaidi waipate fursa hio muhimu.

**Ndugu Wananchi,**

Ilivyokuwa leo tunasherehekea sikukuu ya Idd-el Hajj, ni wajibu wetu tuhakikishe kuwa furaha hii ipo katika familia zetu kwa kula vizuri, kuvaa vizuri na tuiendeleze furaha yetu kwa ndugu na majirani zetu. Hata hivyo, Uislamu umeweka mazingatio maalumu kuhusu kuwapenda watoto kwa kuwapa haki zao na malezi mazuri. Katika kuonesha umuhimu wa kuwajali watoto wetu, imeelezwa katika Hadithi kwamba Mtume Muhammad (S.A.W) ametuhimiza kwa kusema:

***"Wakirimuni watoto wenu na muwafunze tabia njema"***

Kwa hivyo, katika maisha yetu ya kila siku lazima tuwe na mazingatio maalumu kwa watoto wetu kwa kuwahudumia na kuwalea vizuri. Tujitahidi kuwalea na kuwarithisha misingi ya kuheshimu, kukinai na kuthamini vilivyo vyao. Hii ni miongoni mwa misingi ya uzalendo. Vile vile, kuwa na tabia ya kukinai kutawapelekea watoto wetu kutodanganyika kirahisi na kughilibiwa. Marehemu Mzee Abeid Amani Karume katika hotuba zake mbali mbali alikuwa akisisitiza usemi wake maarufu kwamba; *"Tukuza kilicho chako mpaka usahau cha mwenzako".* Tuwafunze watoto wetu maadili mema, silka, desturi na utamaduni wetu tulioristhishwa na wazee wetu; ambao miongoni mwa sifa zake ni kuweza kuishi na watu tafauti na kushirikiana nao katika masuala mbali mbali yenye kheri; yanayohusu maendeleo katika maisha.

An evaluation version of novaPDF was used to create this PDF file.
Purchase a license to generate PDF files without this notice.

Ni dhahiri kuwa wakati tulio nao una harakati nyingi za kimaisha. Hata hivyo, ni wajibu wetu wazazi na walezi kutafuta muda maalumu wa kufuatilia nyendo za watoto wetu na kukaa nao pamoja kuwaeleza kuhusu maisha kulingana na umri wa mtoto. Mwenyezi Mungu anatuonesha mfano katika Surat Luqman, ambapo aya kadhaa katika sura hio zinaonesha jinsi Bwana Luqman alivyokuwa akimuaidhi mwanawe kuhusu mwenendo mwema katika maisha. Watoto wanahitaji malezi

bora. Wasimamiwe, waongozwe, walindwe na wanapokuwa mbali na wazazi wao wafundishwe mikakati ya kujilinda, ili kuwaepusha na mambo yanayoweza kuharibu maisha yao. Mtume (S.A.W) amesema:

> ***"Wafundisheni watoto wenu kwani, wao wamezaliwa katika zama tafauti na zama za aina zenu"*.**

Vile vile, katika kuonesha umuhimu wa wajibu wa wazazi na walezi, kuwapa watoto malezi mazuri imepokewa Hadithi ya Mtume (S.A.W) inayosema:

> **"*Wapendeni watoto wenu na muwahurumie, na mtakapowaahidi (kitu) basi watimizieni, kwani wao hawaoni anayewapatia mahitaji yao ila nyinyi".***

Hadithi hio inatuzindua tuone kuwa tuna wajibu wa msingi wa kuwatimizia watoto wetu mahitaji yao. Kwa hivyo, tujitahidini sana kuutekeleza wajibu wetu huo, kwani watoto ni neema aliyotupa Mwenyezi Mungu.

**Ndugu Wananchi,**

Miongoni mwa mapenzi makubwa ambayo mzazi anawajibika kwa mtoto wake ni kuhakikisha kuwa anapata elimu ya dini na dunia. Kumpa elimu mtoto ni haki yake, ili aweze kupata ufunguo huo muhimu wa maisha.

Tusiache kuyafuatilia maendeleo ya watoto na vijana wetu katika masomo yao skuli na kwenye madrasa. Tuelewe kwamba mzazi au mlezi kuyafuatilia maendeleo ya mtoto wake ni njia mojawapo ya kumpa motisha na ari ya kufanya vizuri katika

An evaluation version of novaPDF was used to create this PDF file.
Purchase a license to generate PDF files without this notice.

masomo yake. Kwa hivyo, tuwafuatilie na tuwahimize wafanye bidii katika masomo yao.

Nawapongeza kwa dhati vijana wote waliofaulu kwa daraja za juu katika mitihani yao ya Kidato cha Sita kwa mwaka 2019. Naamini kwamba wale waliojitahidi na waliojiandaa vizuri ndio wengi katika waliopata matokeo bora zaidi, kwani juhudi ndio shina la mafanikio. Nawapongeza wazazi, walimu na skuli zote zilizofanya vizuri. Nawanasihi wale ambao hawakupata matokeo mazuri wasikate tamaa na watafute namna nyengine ya kujiendeleza. Aidha, naiagiza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, wazitafute sababu zilizopelekea baadhi ya Skuli zetu kuwa miongoni mwa Skuli kumi za mwisho katika matokeo ya mtihani mwaka huu, na hatimae waandae mbinu za ufumbuzi ambazo zitaleta mafanikio hapo baadae.

**Ndugu Wananchi,**

Sikukuu hii inafanyika ikiwa ni takriban wiki sita zimepita tangu vilipomalizika vikao vya Baraza la Wawakilishi, vilivyojadili na hatimae viliidhinisha bajeti za Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020.

Pongezi zangu za dhati nazitoa kwako Makamo wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kwa kusimamia vyema shughuli za Serikali ndani ya Baraza la Wawakilishi. Kadhalika, pongezi maalum nazitoa kwa Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi, Mawaziri na Naibu Mawaziri, Wawakilishi na Wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri mliyoifanya katika kuutekeleza wajibu wenu wa kikatiba. Kwa niaba ya Serikali napenda niwaahidi kuwa Serikali itayafanyia kazi mapendekezo na maoni yaliyotolewa na Waheshimiwa Wawakilishi katika vikao vya Bajeti, kwa lengo la kuleta mafanikio zaidi katika kuwatumikia wananchi wote.

**Ndugu Wananchi,**

Kwa hakika nina furaha kuona kwamba Bajeti Kuu ya Serikali inazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka. Jambo hili linadhihirisha kukua kwa uchumi wetu. Ukuaji wa uchumi unakwenda sambamba na dhamira yetu ya kupanga na kutekeleza mambo

An evaluation version of novaPDF was used to create this PDF file.
Purchase a license to generate PDF files without this notice.

makubwa na muhimu ya maendeleo kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar kwa fedha zetu wenyewe. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, bajeti kuu ya Serikali, imefikia jumla ya TZS trilioni 1.4194 kutoka TZS trilioni 1.3152 kwa mwaka wa fedha 2018/2019, sawa na ongezeko la asilimia 8.0. Sambamba na ongezeko hilo, hatua kwa hatua tunaendelea kupunguza utegemezi wa bajeti, ambapo katika mwaka huu wa fedha wa 2019/2020 umepungua hadi kufikia asilimia 6.7 ikilinganishwa na asilimia 30.2 kwa mwaka 2010/2011.

Matumaini yangu ni kwamba wananchi wengi wamefuatilia majadiliano ya bajeti ya Serikali pamoja na mipango ya Wizara mbali mbali iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha. Napenda niwahakikishie wananchi wote kwamba Serikali imetenga fedha za kutosha, ili kuendelea kutoa huduma za Afya na Elimu bure, kama zilivyoelezwa kwenye Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya mwaka 2015/2020.

Natoa wito kwa wananchi tuendelee kushirikiana na tufanye kazi kwa bidii, ili uchumi wetu ukue kwa kasi kubwa na hatimae tuitekeleze mipango yetu yote kwa ufanisi zaidi. Tumuombe Mwenyezi Mungu atupe nguvu na uwezo mkubwa zaidi wa kupanga na kuitekeleza mipango yetu ya maendeleo kama tulivyoipanga.

Kwa mara nyengine tena, napenda niwakumbushe viongozi na watendaji wote wa Serikali kwamba muongeze kasi, bidii na ari katika kuyatekeleza majukumu yenu ya kuwatumikia wananchi kwa ufanisi kwa kuzingatia bajeti iliyopitishwa na fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka 2019/2020. Tufahamu kuwa, wananchi wana matumaini makubwa kwa Serikali yao, kwa hivyo tuna wajibu wa kufanya kazi kwa bidii, ili tuyafikie matarajio yao. Nina imani kubwa kuwa, uwezo wa kufanya vizuri zaidi katika kuinua uchumi na kuimarisha huduma mbali mbali tunao, iwapo sote tutaitekeleza azma yetu hio. Ni lazima tuongeze kasi ya maendeleo kwa kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa zaidi, kwani huo ni wajibu wetu sote.

**Ndugu Wananchi,**

Wakati tukiwa katika matayarisho ya sikukuu hii ya Idd el Hajj, juzi tarehe 10 Agosti, 2019 tulipokea taarifa ya huzuni ya kutokea kwa ajili ya kuanguka na kuripuka kwa

An evaluation version of novaPDF was used to create this PDF file.
Purchase a license to generate PDF files without this notice.

lori la mafuta katika eneo la Msamvu Mkoani Morogoro na kusababisha vifo vya watu zaidi ya 64 na majeruhi kadhaa. Wananchi wote wa Zanzibar, tunaungana na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro; Dk. Kebwe Stephen Kebwe, wanafamilia, marafiki, wananchi wa Mkoa wa Morogoro na Watanzania wote kwa jumla katika msiba huu mkubwa wa wananchi wenzetu hao.

Kwa hakika huu ni msiba mkubwa kwetu kwa kuwapoteza ghafla Watanzania wenzentu ambao walikuwa ni sehemu ya nguvukazi ya Taifa letu. Tuupokee mtihani huu kwa kuwa na subira na kumwelekea Mola wetu Subhana Wataala kwa kusema; *Inna Lillahi Waina Ilayhi Rajiun*. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awape malazi mema wale waliofariki katika tukio hilo na awape nafuu ya kupona haraka majeruhi wote, ili waweze kuungana tena na familia zao na Watanzania sote katika shughuli mbali mbali za maendeleo. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mhe. Dk. John Pombe Joseph Magufuli ametangaza maombolezo ya siku tatu kuanzia juzi Jumamosi, tarehe 10 Agozti, 2019, ambapo bendera zote zitapepea nusu mlingoti katika maeneo yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa msingi huo, nasi tunaungana na Watanzania wenzetu wote katika maombolezo haya.

**Ndugu Wananchi,**

Namaliza hotuba yangu kwa kukuombeeni nyote kila la kheri katika kuisherehekea sikukuu hii ya Idd el Hajj. Tuisherehekee sikukuu hii kwa kufanya mambo yanayompendeza Mwenyezi Mungu na iwe ni namna ya kumshukuru kwa kutupa neema hii.

Nawakumbusha wale wenye uwezo, kuwa kuchinja mnyama ni miongoni mwa sunna muhimu katika Sikukuu ya Idd ul Adh'ha na nyama hio itumiwe kwa mahitaji ya nyumba zetu, ndugu, jamaa na marafiki zetu, ili sote tuweze kuzishukuru neema zake Subhanahu Wa Taala. Kitendo hiki cha kuchinja na kutoa sadaka kina maana kubwa sana hasa hivi sasa katika kuimarisha udugu, kuhurumiana, kupendana, na kushirikiana katika jamii yetu.

An evaluation version of novaPDF was used to create this PDF file.
Purchase a license to generate PDF files without this notice.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu awajaalie Hijja “mabrur” (Hijja yenye kukubalika) Mahujaji wetu wote na awarudishe nyumbani kwa salama. Mwenyezi Mungu awajaalie wale wote wenye nia ya kwenda kuhiji, uwezo wa kuitekeleza dhamira yao hio. Awape afya njema, ili waweze kuitumia fursa hio muhimu ya kufanya ibada katika mji mtukufu wa Makka na Madina na wapate fadhila kubwa zinazotokana na ibada hizo. Amin.

Kwa baraka za sikukuu hii, tunamuomba Mola wetu aizidishie nchi yetu amani, mapenzi na mshikamano. Atuwezeshe zaidi kuitekeleza mipango yetu ya maendeleo kwa ufanisi wa hali ya juu kwa faida yetu na wale watakaokuja baadae. Mwenyezi Mungu aturudishe nyumbani sote kwa salama na amani.

**Ahsanteni kwa kunisikiliza.**

**IDD MUBARAK**

**KULLU AAMUN WAANTUM BIKHEIR**

An evaluation version of novaPDF was used to create this PDF file.
Purchase a license to generate PDF files without this notice.